## UTANGULIZI

Matazamio ya Taifa liliote katika muda wowote ule yamejengwa juu ya vijana walio chini ya umri wa miaka 25. Vijana hawategemewi katika taifa tu bali na kanisa pia. Kanisa la Waadventista Wasabato katika mtazamo huo, takribani asilimia 50 – 75 ya washiriki wote ni vijana. Kazi ya kanisa kwa vijana ni kufundisha, kuokoa na kuelekeza bidii zao katika mambo ya mbinguni.

Kazi inayowakabili washiriki wa kanisa letu ni kuvutiwa na vijana wetu. Vijana hawa wanahitaji kutiwa moyo, wema, uvumilivu, ukarimu katika kuwahudumia tukijua kwamba shetani anafanya kazi kwa kila dakika kuwavuta katika nyavu zake. C.T 41,42)

Kusudi la kozi hii si tu kuliamsha kanisa kuona umuhimu wa kuwalea vijana, bali kuwasaidia viongozi wa kanisa na vijana wajue namna ya kufanya kazi pamoja na vijana na kuwafundisha njia bora za kutimiza wajibu wao wa injili.

Kanisa ni lazima litambue kwamba vijana si wa muhimu kwa ajili ya baade tu, lakini ndio wenye nguvu za pekee kwa ajili ya kutumika. Kanisa linawahitaji vijana na wao wanalihitaji kanisa.

## UMUHIMU WA VIJANA KATIKA KANISA.

**1. Vijana huleta mwamko katika kanisa:**

"Kanisa linahitaji sana vijana ambao watabeba ushuhuda kwa ujasiri ambao moto wao utaamsha nguvu za watu wa Mungu na hivyo kuongeza nguvu ya kanisa katika ulimwengu"(*MYP pg 25)*

**2. Vijana wana mvuto wa kipekee:**

Shetani anaelewa vizuri kwamba hakuna umri mwingine unaoweza kufanya mema na makuu kama vijana wa kiume na wa kike waliojitoa wakfu kwa Mungu. Vijana kama wako sahihi wanaweza kuwa na mvuto wa pekee. (Ibid 204)

- ❖ Wahubiri, washiriki (laymen) wenye miaka mingi kazini hawawezi kuwa na hata nusu ya mvuto kwa vijana waliojitoa kwa Mungu kama ambavyo wanaweza kuwa na mvuto kwa vijana wenzao. (ibid 204)

**3. Vijana wanahitajika kumaliza kazi ya Mungu:**

Kama jeshi la watenda kazi la Vijana wetu wakiwa wamefundishwa vizuri watakwenda haraka ni kwa haraka kiasi gani ujumbe wa Msulubiwa aliyefufuka na ajaye haraka atachukuliwa katika ulimwengu wote. (ibid 196)

**4. Vijana wanahitajika katika kupamba na kubuni kazi:**

Ili kazi iende mbele katika matawi yote, Mungu anawaita vijana wenye moto na ujasiri. Anawachagua vijana kupanga maendeleo ya kazi yake. Vijana wa kike na wa kiume wanaalikwa katika kuimarisha kazi ya Mungu kwa juhudi na mwamko wa kipekee. Kwa njia hiyo wataleta utukufu kwake na wokovu kwa wanadamu wenzao. (Gospel Workers 67)

## NGUZO SABA ZA IDARA YA VIJANA

Kanisa la Waadventista wasabato lina nguzo/imani za Msingi 28, ambayo mafundisho makuu ya Biblia yamejengwa. Hali kadhalika katika Idara ya vijana kuna nguzo kuu Saba zinazoongoza na kusimamia mambo kadhaa ya chama bila kuathiri imani za Msingi za kanisa.

**Nguzo hizo ni:**

1. **MUUNDO WA IDARA:** Nguzo hii huwakilisha historia na muundo wa huduma za Idara ya Vijana katika kanisa letu.
2. **UONGOZI:** Hii hufundisha falsafa ya uongozi katika kanisa la Waadventista Wasabato, mkazo ukiwa katika aina ya viongozi wanaohitajika, saikolojia ya uongozi na kazi zake na jinsi ya kuendesha kamati za chama
3. **KUJITOA:** Nguzo hii inakutaka uelewe kwamba shughuli zote katika chama cha vijana zinahitaji Kujitoa kikamilifu. **Uhusiano na Mungu** unapaswa kukuzwa katika chama kwa njia ya majuma ya maombi, vipindi vya uamsho, mikono ya kujifunza kweli za Biblia, maombi ya asubuhi, ya binafsi na ya kifamilia)

- Nguzo hii ipo ili kuimarisha maisha ya kiroho ya vijana na viongozi wao.

4. **UANAFUNZI:** Nguzo hii inawasaidia vijana namna ya kuwa wanafunzi wa Yesu, na kuyafanya maisha yao kuishi kwa ajili yake. Kila kijana anapaswa kuwa mwanafunzi wa Yesu kwa kujifunza maandiko na kuishi kulingana na yale anayojifunza.
5. **IBADA:** Ibada si ile ya kuhudhuria kanisani tu ama ile ya nyumbani. Ibada ni kujifunza namna ya kuishi pamoja na Mungu na kuhusianisha mafunzo hayo na maisha yako ya kila siku.
6. **KUSHUHUDIA:** Nguzo hii inamtaka kila kijana kushirikisha maarifa yetu ya kumfahamu Mungu kwa wengine. **Mathayo 28:18 - 19, Marko 16:15 – 16, Warumi 10:14.**
7. **USHIRIKA:** Hii inahusika na kutoa maburudisho yafaayo kwa vijana. Ushirika unahusisha nyimbo, ziara za mafunzo, michezo, kambi za mafunzo,

mikutano ya kujifunza Biblia(*Bible Conferensi*), rally, nishani, pini, ugunduzi wa viumbe asili,okoa jamii n.k.

## MUUNDO WA IDARA YA VIJANA

### A: HISTORIA YA CHAMA CHA VIJANA

***Mwanzo wa idara ya vijana katika Biblia. Kutoka 10: 9***

Idara ya vijana (chama cha vijana) imeanzishwa katika kanisa la SDA mwaka **1879,** ambapo vijana **Harry Fenner** akiwa na umri wa miaka 16 na **Luther Warren** akiwa na miaka 14 walipoitisha mkutano kule **Hezilton Michigan** huko **Marekani.** Mkutano huo uliwahusisha vijana wa kiume peke yao na ulifanyika katika chumba kidogo ndani ya nyumba ya wazazi wa Luther Warren.

**MAKUSUDI YA MKUTANO HUO:** kusudi kubwa la mkutano huo ulikuwa ni kuhamasisha kazi ya Umishionari na kupata fedha kwa ajili ya vijizuu. Baadae vijana wa kike walikaribishwa kujiunga na mikutano hii ya vijana ambayo ilitafutiwa mahali pakubwa ambapo wazazi walikaribishwa kuhudhuria.

Historia inasema baraza la kanisa na wazazi walijadili namna wanavyoweza kuwasaidia vijana wao kuwa wamishionari. **Ndg. Fenner** pamoja na vijana wengine waliokuwa na moto wa injili waliombwa kuwasaidia na kuwatia moyo vijana wenzao kuipenda kazi ya Mungu. Ujumbe wa malaika wa 3 ulitimizwa hapa.

**Ellen G. White** Disemba 19, 1892, aliandika ujumbe kwa kanisa juu ya wajibu wao wa kufanya jambo fulani kwa ajili ya vijana akiwa Australia. "Tunalo jeshi la vijana leo ambao wanaweza wakafanya makuu ikiwa wataelekezwa vizuri na kutiwa moyo. Tunahitaji watoto wetu wauamini ukweli.Hebu waelimishwe ili wauwakilishe ukweli mahali popote watakapoitwa kutumika".*(General Conference Bulletin January 29, 30, 1893 pg 24)*

Vijana wa kiume na wa kike, anzisheni vikundi kama askari wa Yesu. Jiandikisheni kazini, wekeni nguvu, ujuzi na talanta zenu katika huduma ya Bwana wenu ili kuokoa roho zinazopotea. Hebu kuwe na vikundi vilivyoanzishwa katika kila kuifanya kazi hii. ***(Sign of the times May 27, 1893).***

Kwa kuitikia wito huo, vikundi mbalimbali vilivyounda umoja wa vijana vilianzishwa makanisani. Kwa mfano:

- Mwaka 1891 chama cha vijana kilianzishwa huko Antingo, Wisconsin (Ulaya)
- Mwaka 1893 chama kilianzishwa huko Lincoln, Nebraska (Ulaya)
- Mwaka 1894 vikosi vya injili vya vijana vikaanzishwa na Luther Warren huko South Dakota.

Mwaka **1901** General Conference ikachukua hatua ya kuanzisha chama cha vijana rasmi. Baraza likamchagua mkurugenzi wa Shule ya Sabato **Mrs. Plummer** kusimamia chama cha vijana. Baadae **1907** baraza la G. C. Lililokutana kule Gland, Seitzealand likamchagua **ndugu M.E. Kern** kuwa mwenyekiti wa vijana na mama **Matilda Erickson** kuwa katibu wa chama.

Mwaka 1907 jina rasmi likachaguliwa, jina **M.V (Missionary Volunteer)** yaani vijana watakaofanya kazi ya umishenari kwa njia ya kujitolea. Ndipo chama kikapewa hadhi ya kuitwa idara ya **Missionary Volunteers.** (M.V)

Mwaka 1946 Ndg John Hancock aliendesha conference ya kwanza ya watafutanjia huko Califonia. Kuanzia mwaka 1947 hadi 1950 programme za watafuta njia ziliendelea kukua katika Union Conference ya Pacific. Baadae general Conference **ikaanzisha rasmi chama cha watafuta njia mwaka 1950.**


Katika mwaka 1972 jina likabadilishwa kuwa Youth Department of Missionary Volunteers yaani idara ya vijana ya wamishenari wa kujitolea. **Mwaka 1978** jina likabadilishwa kuwa **Adventist Youth** yaani Vijana wa Kiadventista.

**B. MUUNDO WA IDARA YA VIJANA**


Idara ya Vijana inaundwa na vyama vinne katika kanisa. Navyo ni:

1. Vijana wakubwa wa AY ( Adventista Youth) miaka 16 – 35+
2. Vijana Mabalozi (Christ Ambasodor) miaka 16 – 21
3. Vijana wadogo wa Watafuta – Njia (Pathfinders) miaka 10 – 15
4. Vijana wadogo wa Wavumbuzi (Adventures) miaka 4 – 6

## MUUNDO WA IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA




### MUUNDO WA IDARA YA VIJANA KANISANI



**Maelezo ya uanzishaji wa vyama.**

- Chama cha vijana wakubwa kilianzishwa mwaka 1879
- Chama cha mabalozi kimeanzishwa mwaka 2001
- Chama cha watafutanjia kilianzishwa mwaka 1950
- Chama cha wavumbuzi kilanzishwa mwaka 1939
    - **Kila chama kina madarasa na vikosi kazi.**

## MALENGO YA IDARA VIJANA

**Malengo:** Roho ya Unabii inaweka makusudi ya kuwa na chama cha vijana kanisani kama ifuatavyo:

1. Kuwaelimisha vijana kufanya kazi kwa ajili ya vijana wanaoitunza Sabato
2. Kuwaelimisha vijana kulisaidia kanisa na wale wote wanaoitunza Sabato.
3. Kufanya kazi kwa ajili ya watu wasio wa imani yetu(*wasio waadventista Wasabato)* Signs of the times, May 29, 1893
    - **Rejea: Message to young People pg 208, 204, 207, 220**
    - **Kanuni ya Kanisa sura ya 9 uk 18**

**KATIKA KUTIMIZA MAKUSUDI HAYA VIJANA;**

Zaburi 133:1, Yohana 17:11 – 21, Waefeso 12, 13.

- Nia ni kujenga jeshi la Vijana wenye umoja thabiti katika Kristo ili kumfanyia kazi na kuufikia ufalme wa Wake
- Wataomba pamoja
- Watajifunza neno la Mungu pamoja
- Watashirikiana pamoja
- Watakutana katika vikundi vidogovidogo kupanga namna ya kushuhudia
- Kukuza mbinu, ujuzi na talanta katika kumtumikia Bwana
- Kutiana moyo katika kukua Kiroho

NB: Kama haya hayafanyiki, kanisa litakuwa limepoteza njozi

**MWELEKEO WA IDARA YA VIJANA**

**LENGO:** Kuokoa kutoka dhambini, na kuelekeza katika utumishi

**KUSUDI:** Habari njema ya ufalme ihubiriwe ulimwenguni kote katika kizazi changu. Mathayo 24:14

**MOTTO:** Kwa maana upendo wa Krsito wanibidisha. 2Wakorintho 5:14

**AHADI:** Nikimpenda Bwana Yesu, Naadhidi kuchukua sehemu ya juhudi katika chama cha vijana wajitoleao kumtumikia Kristo,Kufanya yote niwezayo, kuwasaidia wengine, Na kuimaliza kazi ya injili ulimwenguni kote.

**WIMBO WA CHAMA:**

**Oh! AY Mashahidi wa Yesu, chama kizuri chenye kusudi kubwa, kinatupendeza vijana wa kiume pia wa kike oh! AY mashahidi wa Yesu**

**Tuna ahadi nasi tunaitunza katika kazi sisi hatuogopi Yesu ametutuma leo tueneze injili yake Oh! AY mashahidi wa Yesu**

**SERA/ MAMBO YANAYOENDESHA IDARA**

1. Mambo ya fedha
2. Sare

**MAOFISA WA CHAMA CHA AY**

Kila chama lazima kiwe na maofisa wanaochukua majukumu ya kupanga na kusimamia kazi. Kuna maofisa wa aina mbili.

1. Wanaochaguliwa na kamati (baraza la) ya uchaguzi
2. Wanaochaguliwa na wanachama wenyewe.

**A.Wanaochaguliwa na baraza la uchaguzi**

- Mkurugenzi/ Kiongozi wa vijana
- Kiongozi mwenza
- Katibu/ Katibu Mhazini

- Katibu Mhazini msaidizi
- Mdhamini au Mshauri wa Vijana

NB: Ikiwa wanachama ni wachache, nafasi mbili zaweza kushikwa na mtu mmoja.

**B.Wale wanaochaguliwa na wanachama wenyewe**

- Kiongozi wa Mawasiliano
- Kiongozi wa Kwaya ya chama
- Kiongozi wa Elimu
- Kiongozi wa maburudisho ya Kikristo
- Kiongozi wa Uinjilisti/Kiroho
- Kiongozi wa Nidhamu
- Mkuu wa Miradi

**UANACHAMA**

- Vijana wote wa kanisa kati ya miaka 16 – 35 wanaweza kuwa wanachama wa AY.
- Wanapojiunga na chama wanapaswa kuahidi ahadi ya AY.

**AINA ZA WANACHAMA**

Kuna wanachama wa aina tatu.

1. **WANACHAMA WA KAWAIDA:** Vijana wenye umri kati ya miaka 16 – 35$^{+}$, ambao ni waadventista wasabato walio na msimamo na mwenendo safi na ambao wanayakubali malengo ya chama, nawanahiari ya kumfanyia Yesu kazi wajiandikishe katika chama.

2. **WANACHAMA SHIRIKISHI:** Hawa ni vijana ambao sio Waadventista Wasabato lakini wenye mitazamo ya Kikristo na wanaopenda kushirikishwa na vijana wa kanisa katika kazi ya utume wanakubaliwa

kuwa wanachama.(***Ndio sababu tuna kwaya ya Vijana kwa ajili ya watu kama hao.)***

- Hawa hawapewi madaraka yoyote ila watiwe moyo kuwa wanachama wa kawaida kadri inavyowezekana. Ikiwezekana washawishiwe kubatizwa.

3. **WANACHAMA WA HESHIMA:** Hawa ni watu wazima ambao umri wao umepita umri wa ujana, lakini bado wanapenda kufanya kazi za umishionari na kupenda mikutano ya vijana wanakubalika na kupokelewa kama wanachama wa heshima.
   - Wanachama hawa hawajumuishwi katika taarifa ya katibu. Wao hutoa taarifa ya utendaji kwa njia ya kawaida kanisani.
     *Kanuni ya Kanisa Toleo la 17, 2005 sura ya 9, uk 52 – 53*

**PROGRAM ZA VIJANA.**

Kuna mikutano ya kawaida ya kila wiki.Hii inahusisha yafuatayo:

i. **Mikutano ya uzoefu:** Kupata uzoefu kutoka kwa watu binafsi kutoa visa walivyopata katika kumfanyia Mungu kazi. Visa vya uinjilisti, shuhuda mbalimbali n.k
ii. **Mikutano ya kiroho:** Kujifunza neno la Mungu. *Mfano*; unabii, kuomba pamoja, mada mbalimbali za Biblia zilizochaguliwa.
iii. **Mikutano ya kuongeza ujuzi:** Mafunzo ya nishani mbalimbali, vipawa, kilimo, bustani, kozi za master guide na kiongozi mwadventista n. k
iv. **Mikutano ya maburudisho ya Kikristo:** Nyimbo, michezo iliyochaguliwa vizuri, vitendawili, hiking, camping, chotto n.k
v. **Mikutano ya uamsho:** Rallies, Bible conference,
vi. **Mikutano ya Uinjilisti:**Juma la maombi ya vijana, effort, kuwatembelea wanaolegea na wanaorudi nyuma, uamsho, kuhudumia wahitaji.

**MIKUTANO YA KANISA, MTAA, KANDA, KONFERENSI, UNION, GC**

Hii ni mikutano inayoandaliwa inayokutanisha vijana kutoka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali ya kiroho na stadi za maisha.

**MAMBO YA KUZINGATIA UNAPOANDAA PROGRAMME.**

- Programme ziwe nzuri zinazoimarisha chama, zikiwa za kulegalega huweza kuhafifisha idara na huweza kukatisha tamaa.
- Yesu awe kiini cha kila programme.
- Programme zisiwe za kuburudisha tu bali za kuwaandaa vijana kutumika
- Programme zisiwe za kujirudiarudia. Kuwe na mambo mapya.
- Ni sehemu ya kugundua talanta na karama mbalimbali za vijana,kwa hiyo ni lazima kuwe na ubunifu wa mambo.
- Wagawie vijana sehemu ya kufanya na uwatake kuleta mawazo ya kuboresha.
- Tumia miongozo mbalimbali kuandaa programme.

❖ **Umuhimu mkubwa wa Vijana ni kumtumikia Kristo na kutenda wajibu wao kama wafuasi na wanafunzi halisi wa Yesu**

## UONGOZI WA KIKRISTO

- Neno Kiongozi, limechukuliwa kutoka neno la Kijerumani lenye maana ya kuwezesha kwenda.
- Ni katika mfano huohuo limetumika katika lugha ya kiingereza likionesha kuongoza, ama kuonesha njia kwa vitendo.

**Kiongozi ni nani? Ni yule:**

i. Anayefanya mambo yaende kwa utaratibu
ii. Anayetoa maelekezo
iii. Anayeonesha njia sahihi
iv. Anayebeba mizigo. Kutoka 18:22
v. Kiongozi ni yule anayetafuta ufumbuzi wa matatizo na si kulalamika.

**Uongozi wa Kikristo ni uongozi wa jinsi gani?**

i. Ni kuteseka kwa ajili ya wengine; Waebrania 13:17, 1Wathesalonike 5: 12 – 13
ii. Uongozi wa Kikristo ni kutumika; Mathayo 23: 11, 20: 26 -28
iii. Ni kujitoa; Warumi 12:1, Mwanzo 12:1
iv. Ni kuwa na moyo wa bidii; Yoshua 1: 6 - 9
v. Ni kuwa na uwezo wa kuongoza: Kutoka 18:21
vi. Ni kuwa na uwezo wa kuwavuta wengine na kuwatia moyo. *(si mwenye kukatisha tamaa)Yohana 12:32*
vii. Wito kutoka kwa Mungu: 2Timotheo 2:15
viii. Wito Mtakatifu: Kiongozi umeitwa kwa kazi Takatifu. Mbingu zitakutumia kuwandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Hivyo tunapaswa kusema kama Paulo (Matendo 9:6) "Niambie yanipasayo kutenda"
ix. Ni mbebaji wa mizigo: Katika amani, furaha, magonjwa na matatizo ya kila namna yatakufanya uwe na uzoefu zaidi kumfanyia Mungu kazi. Kiongozi anapaswa kuchukua kila aina ya jukumu zito na jepesi kwa watu anaowaongoza.

x. Uongozi wa Kikristo unahitaji kujifunza: Kiongozi anapaswa kujifunza na kujiendeleza zaidi kwa kuhudhuria semina za uongozi na kusoma vitabu. "Mafunzo yanahitajika kadri unavyokubali wito wa kumfanyia Mungu kazi."

- *Unapoulizwa kuwa kiongozi wa vijana ni lazima ujiulize shughuli kubwa ya Idara ya Vijana katika Kanisa la Waadventista Wasabato ni nini. Ni kuwandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Hili ndilo jukumu kubwa, na shughuli kuu ya idara ya vijana.*
- *Hivyo basi, lolote tupaswalo kulitenda kwa ajili ya kuwatumikia vijana wa kanisa yatupasa tufanye sasa.*
- *Mungu amekupa nafasi ya Uongozi. Anatazamia kuyatumia madaraka kwa manufaa ya vijana na kanisa kwa ujumla.*

**SIFA ZA KIONGOZI**

1. Awe mwaminifu, mkweli, mvumilivu nawa haki katika mambo yote ya kimwili na kiroho, mwenye msimamo wa kuitetea kweli wakati wote.(ikiwezekana kufa kuliko kuiasi sheria ya Mungu) **Ufunuo 2:10, Kutoka 18:21, 2Timotheo 2:15**
2. Awe anapenda sana mambo ya Kiroho, kusoma Biblia, Roho ya Unabii na Kanuni ya kanisa na kuvifanya kuwa mwongozo wake,kuhudhuria vipindi vya ibada. Ezekiel 2:8 – 3:3, Matendo 17:10 - 11
3. Awe anawapenda vijana na kuwafanya rafiki zake, kuwatembelea, kuwatia moyo na kuomba nao.
4. Si mwenye kutumia nguvu kushurutisha mambo, bali mwenye kutumia busara na ushawishi.
5. Awe mwenye kushirikiana nao katika mambo mbalimbali, na kuandamana nao mahali waendapo.
6. Awe na msimamo katika maamuzi na mwenye kusimamia vema yale yanayotakiwa kufanyika ama yaliyokwishaamuliwa.

7. Mwenye kuelewa mabadiliko ya vijana. *(asiwe na wasiwasi katika mabadiliko hayo)* Mfano vijana wanapobarehe, kuvunja ungo n.k
8. Awe mwenye kuhimizamara zote juhudiya kazi. Si mwenye kuendekeza mambo ya kivivu na ulegevu.
9. Awe mwenye kushukuru kwa kila jambo linalofanywa na vijana na kuwapongeza. 1Wathesalonike 5:18
10. Awe mwenye kubadilisha mambo ya kufanya/ awe mbunifu
11. Ajue kupanga majukumu na kugawa madaraka. Awaamini wale anaofanya nao kazi. ***Kutoka 18, Hesabu 13: 1 - 3***
12. Awe mwenye kushirikiana na viongozi wengine wa kanisa. Mfano Wazee, Mchungaji, Maofisa wengine n.k
13. Awe mwenye kutoa msaadawakati wowote anapohitajika
14. Awe anaipenda kazi ya uongozi,ila asiwe na tamaa ya madaraka
15. Asiwe mwenye kukubaliana na mambo manyonge ili kuwapendeza vijana, ilihali yanakwenda kinyume na imani
16. Asiwe mwenye kukatisha tamaa moyo wa vijana katika kutendajambo jema. Mfano, ubunifu, vipaji, kuimba, mafunzo mbalimbali nk.
17. Mwenye kuandaa wengine kuwa viongozi
18. Asiwe mtu mwenye kujenga makundikwa namna yoyote ile. (rangi, elimu, mali, cheo, talanta n.k)
19. Si mwenye kuwaaibisha na kuwadhalilisha vijana.
20. Mwenye kukubali makosa, kukosolewa na kurekebishwa na aliye tayari kuomba msamaha
21. Asiwe mlalamikaji bali mwenye kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyopo.
22. Asiwe mwenye kulaumiwa au kutuhumiwa na kupenda mapato ya aibu na tuhuma. 1Timotheo 3:7,8

**KAZI/MAJUKUMU YA KIONGOZI**

1. Kusimamia na kusaidia kukuza hali ya kiroho kwa watu anaowaongoza
2. Kuwatunza watu Kiroho na Kimwili, kwa kuwalisha neno la Mungu, na kuwafundisha
3. Kujengamahusiano mazuri miongoni mwa wale anaowaongoza
4. Kupanga na kusimamia malengo ya idara husika kama yalivyopangwa na kuyatekeleza.
5. Kuwapenda watu wote, kuwaonya na kuwakemea. 2 Timotheo 3:16, Tito 2:6 - 8
6. Kushirikiana nao katika matatizo na furaha zao
7. Kufuata mfano wa Yesu wa utendaji
8. Kutuma taarifa kwa Mchungaji wa Mtaa
9. Kuelekeza yalemema yote yaliyokusudiwa.
10. Kuwapa nafasi ya kufurahia ushirika wa kuishi katika Kristo (***to enjoy Christian fellowship) Wafilipi 4: 4***

**MIIKO YA UONGOZI (ETHICS)**

1. Ni mwiko kwa Kiongozi kujiona bora kuliko wengine. Wafilipi 2:3,4
2. Ni mwiko kutumia juhudi za Vijana kujinufaisha mwenyewe
3. Ni mwiko kuacha mambo yazorote na hali ukijutia kwamba yanazorota
4. Ni mwiko kuonesha mashaka kwa wale unaowaongoza
5. Ni mwiko kutenda kinyume na unavyosema
6. Ni mwiko kutamka maneno ya kukatisha tamaa hata kama unafahamu kwamba kuna tatizo.
7. Ni mwiko kutoa siri za watu unaowaongoza.
8. Ni mwiko kufanya mambo bila maandalizi mazuri. *(mfano kufundisha, mambo mbalimbali ya vijana)*

## MFANO WA YESU WA UONGOZI

### A: MAISHA YAKE NI MFANO WA KUUISHI.

- Alivyofundisha na alivyosema ndivyo alivyoishi. "Nimewapa kielelezo mtende kama nilivyotenda mimi"Maneno ya Kristo yalikuwa kielelezo kamili kwa mtu yeyote yule.Yesu alifundisha kweli kwa kuwa yeye mwenyewe ndio kweli. Mambo hayayalifanya mafundisho yake kuwa na nguvu.
- Wengi walimwendea Yesu na kurudi na taarifa kwamba hakuna kamwe mtu aliyezungumza kama yeye.Hakuna mwanadamu aliyeishi kama Yesu na ikiwa maisha yake yangelikuwa kinyume asingeweza kuzungumza kama alivyokuwa akifanya. (M.H 469)

### B: ALIJALI NA KUELEWA MAHITAJI YA WENGINE

- Akawa mmoja na sisi na mmoja wetu na alielewa udhaifu wa ubinadamu (waebrania 2: 17, 14:15 – 16)
- Maisha yake yaliongozwa huku yakijazwa na upendo na mbingu zilikuwa juu yake zikitoa maana kwa kila alilozungumza (ST 253)

### C: ALIKUWA MWEMA NA MWENYE UPEO WA MAWAZO

- "Kama Yesu atakaa ndani yetu, tutakuwa wavumilivu, wema, wachangamfu na watendaji" (ST 253)

### D: ALIMWONA KILA MMOJA MTAHINIWA WA MBINGUNI

- Mara kwa mara alikutana na walio chini ya uongozi wa shetani na ambao hawana nguvu ya kuvunja minyororo yake. Kwa wale ambao walikata tamaa, wagonjwa, waliojaribiwa walioanguka n.k. Yesu alizungumza nao maneno ya faraja, yaliyohitajika na yaliyoeleweka kwa wahitaji. Alikutana na wengine waliokuwa wakipigana vita ya Kiroho. Hawa aliwatia moyo na akiwahakikishia ushindi na kwamba Malaika wa Mungu walikuwa upande wao na wangewapatia ushindi. (MH 26)

**E: ALIKUWA NA MZIGO WA UMISHIONARI**

- Yohana 18:37, Luka 2:49. Kazi za Baba yangu
- Yesu alichukua uzito wa majukumu kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Alifahamu umuhimu wakuwa na mabadiliko ya kanuni na makusudi ya mwanadamu vinginevyo wote watapotea. Huu ndio ulikuwa msingi waroho yake. (MH 14, 18)

**F: ALIKUWA MNYENYEKEVU NA ALIMTEGEMEA BABA WA MBINGUNI**

- Yohana 5:30
- Mwana wa Mungu alijitoa kwa matakwa ya Baba yake na alimtegemea. Alikubali mipango ya Mungu kwa ajili yake. *(Desire of Ages 208)*

**G: ALITOA MUDA WAKE WOTE KWA KUONGOA ROHO**

- Njia pekee alizotumia Yesu zitatupatia mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mkombozi alijichanganya na watu kama mmoja aliyehitaji bidhaa zao. Alionesha wema wake kwao, alishughulikia mahitaji yao. Ndipo aliwafanya wamfuate. (hakikisha unapojichanganya uwe umevaa silaha za Kristo.)

**Muhtasari:** Yesu alijishughulisha sana na mawazo na maisha ya watu ili aweze kupata mioyo yao. Na kwamba ajaze fikra zao kwa chakula cha Kiroho na kile cha kimwili. *(mfano alipolisha watu 5000)*.

- Wengine walimfuata kwa sababu walipewa chakula na hivyo aliwapata
- Alitoa faraja kwa waliofiwa na wapendwa wao na wengine aliwafufua. Aliponya magonjwa ya kimwili na kiroho.
- Mambo aliyoyafanya Yesu ni muhimu kwa kila Kiongozi ili aweze kujifunza shughuli zote njema zinazomhusu binadamu kujua mahitaji yao na kuwasaidia.
- Yesu aliponya mwili kisha roho. Vivyo hivyo nasi kama viongozi na washiriki tunao wajibu wa kufuata kanuni hiyo.

**WITO:** Watenda kazi wa Yesu wanaofanikiwa katika juhudi zao wanapaswa kumfahamu Kristo. Kule mbinguni kufaa kwao kama watumishi hupimwa kwa uweza wao wa kupenda kama Kristo alivyopenda na kufanya kazi kama alivyofanya. ( AA 530, 551)

**CHANGAMOTO KATIKA UONGOZI**

1. **KIONGOZI NI KAMA DIRA**: Kiongozi akisema jambo watu hufuata ama kutekelezakama agizo lilivyosemwa.

- Kiongozi aweza kukosea na aweza kukosolewa na wachache lakini wengine wakibaki wananung'unukia chinichini.
- Unapogundua umekosea ama watu unaowaongoza, ni wakati wa kutafakari jambo hilo na kurudi katika msitari la sivyo utawaongoza katika upotevu.

2. **WATU WANAKUTEGEMEA KUTOA ZAIDI YA ULICHONACHO**

- Kiongozi anaaminika kuwa na nafasi ya kuwafikia watu na kuwasidia kwa hali na mali. Wakati mwingine aweza asiwafikie ama kuwasaidia wote. Jambo hili laweza kukuleta shida. Kwa hiyo unapaswa kulikabili kwa upole na busara za mbingu.
- Kuna wakati ambapo walio chini yako watazua matatizo na kukuachia uyatatue mwenyewe, inakupasa uyakabili.
- Utapewa lawama nyingi na kwa nyakati tofauti. (ikiwa tuhuma unazotuhumiwa ni za kweli na ikiwezekana uachie madaraka)

  *(Kiongozi hapaswi kulaumiwa kwa mabaya na tuhuma za madeni, wizi, uasherati, ulevi n.k)*
- Waweza pia kusifiwa ingawa sifa huwa chache na zingine za kinafiki.

  *Kuna usemi usemao "***Matatizo ni mkate na siagi ya uongozi".** Ukiwa kiongozi unategewa kujitoa kafara, kuumia ikibidi kufa, kuteseka kwa ajili ya wale unaowaongoza. Warumi 5:9. Usikate tamaa wala kuogopa kwa sababu Roho wa Mungu yuko pamoja na wewe. **Joshua 1:6 – 7, 9**

**3. WATU KUTOKUWAJIBIKA**

- Kuna wakati ambao watu hawatimizi wajibu wao katika utendaji na mara zingine hata viongozi wenzako wanazorotesha mambo. (Kutatua tatizo hili peleka taarifa kwa viongozi wa juu na washauri wa vijana.

**HATUA ZA UTENDAJI KATIKA UONGOZI**

1. **Kupanga:** Kiongozi lazima awe mwenye njozi na mipango inayoeleweka na mwenye kufuata ratiba. Anapaswa kuileta mipango hiyo kwenye baraza la vijana ilikuitathmini na kuiboresha kwamba itekelezwe au la.
2. **Kuelimisha:** Kiongozi anapaswa kuwaelimisha watu wake juu ya jambo fulani ama mipango iliyopo.
3. **Kutekeleza:** Kiongozi anao wajibu wa kutoa matokeo juu ya mipango iliyopo kwa kutekeleza na kusimamia malengo ya idara.
4. **Kutoa Taarifa (Tathmini):** Kiongozi anapaswa kutoa taarifa ama tathmini ya utendaji wa mambo mbalimbali kwa kadri inavyokubaliwa kutolewa. Taarifa inaweza kutolewa kwa mwezi, robo au kwa tukio ambalo taarifa yake inahitajika haraka. ***(Kazi bila taarifa ni sawa na kutabasamu gizani)***

***(*Kipimo cha uongozi ni jinsi anavyoweza kuleta ushawishi kwa watu na kufikia maendeleo bora.)***

**KANUNI YA MAFANIKIO KATIKA UONGOZI**

1. **Malengo yawe wazi**

- Malengo, bajeti na mipango lazima viwe wazi kwa wanachama
- Kuitisha mikutano ya mara kwa mara na kuwe na sababu za msingi za kuwakutanisha watu.

2. **Weka Mipango**
    - Mikutano mizuri haitokei kama ajali. Inahitaji muda, juhudi na mipango madhubuti. Weka mipango vizuri na ieleweke, simamia na kutekeleza mipango

3. **Kuweka Juhudi katika utekelezaji**
    - Kuwe na juhudi ya kuwandaa vijana katika kutekeleza majukukumu yao ya kiidara
    - Himiza wanachama kuchangia gharama za uendeshaji wa kazi za idara.
    - Juhudi nyingi katika mipango huleta matokeo mazuri
4. **Tangaza:**
    - Tangaza mikutano ya vijana hadharani na ieleweke kwa wote na kwa muda unaokubalika
    - Kama huna jambo la kuvutia usiitishe mkutano wala vikao.
5. **Wepesi**
    - Uwepo wepesi wa kuanza na kumaliza mambo kwa wakati.
6. **Ushiriki(Participation)**
    - Hakuna jambo litakalofaulu ikiwa wanaoshiriki ni viongozi au watu wachache tu.
    - Himiza vijana kushiriki kwa ufasaha katika mambo ya kiidara na kila mmoja ajue anahusika katika jambo fulani.

**MIFUMO / AINA ZA UONGOZI**

Kuna aina nyingi za mifumo ya uongozi

1. **Democracy:**
    - Huu ni utawala wa umma kwa manufaa ya umma. Watu hupewa nafasi ya kuamua mambo na kuchagua kwa hiari yao wenyewe kile wanachokihitaji.
    - Kuna hali ya kukosoana na kupongezana miongoni mwa watu
    - Kuna uwajibikaji miongoni mwa wanachama na uongozi
2. **Uongozi wa Kiimla (Kidikteta)**
    - Unatumia amri (mabavu) katika kuamua ama kuagiza mambo.
    - Amri zinatoka juu kuja chini

- Kiongozi anawagawa wanachama na yupo kwa maslahi yake ama ya kundi fulani lenye nguvu kifedha n.k
- Maslahi ya wanachama hayapewi uzito
- Hauko wazi juu ya mapato na matumizi
- Hauruhusu kukosolewa au kushauriwa

3. **Uongozi huria/ huru**
    - Kiongozi hana mamlaka, kila mtu anafanya anavyotaka
    - Maamuzi yanatolewa na yeyote yule.
    - Ufanisi katika kazi huwa mdogo kwa kukosekana usimamizi madhubuti.
    - Kila mtu anamlaumu mwenzake
    - Ubadhirifu wa rasilimali huwa mkubwa
    - Unazalisha majungu na vikundi visivyoleta maslahi kwenye chama,na unadhoofisha nguvu na uhai wa chama ama jumuiya.

**JINSI YA KUENDESHA IDARA YA VIJANA**

Kiongozi anapaswa kufanya nini ili aweze kuendesha Idara ya Vijana

1. **Ipende kazi.**
    - Uwe na mawazo chanya, ifanye kwa moyo bila kutegea wala kutaka sifa.
2. **Jishughulishe kupata maarifa mapya.**
    - Soma vitabu vya Kiada na ziada kupata maarifa mapya.
3. **Hudhuria semina mbalimbali.**
    - Inakupasakuhudhuria semina zinazoandaliwaField/Conference au ngazi za juu za kanisa, mtaa na kanisa mahalia.
    - Semina zitakusaidia kujua mambo mbalimbali yahusuyo kanisa na taasisi zake, pamoja na mabadiliko yoyote yaliyopo kwa wakati huo.
4. **Jenga uhusiano mzuri na viongozi wa kanisa**
    - Shirikiana na viongozi, na wanachama, kuandaa yale mnayokusudia kuyafanya katika chama chenu.

- ❖ Ongea na viongozi wa kanisa ili upate mawazo yao, na wao wapate mawazo yenu kabla ya baraza la kanisa halijaketi.
- ❖ Hili litarahisisha kazi ya kuzifafanua agenda zako kwenye baraza; maana uongozi wa kanisa utakusaidia.

**5. Omba ushauri.**

- ❖ Kwa viongozi wa kanisa
- ❖ Kwa washiriki wenye uzoefu
- ❖ Kwa viongozi wenzako waliokutangulia
- ❖ Kwa wanachama unaowaongoza.

**6. Kubali kushauriwa na kukosolewa**

- ❖ Tambua kwamba, hakuna binadamu aliyemkamilifu.
- ❖ Kiongozi si rahisi kuona makosa yako isipokuwa watu unaowaongoza au wanaokuzunguka
- ❖ Epuka kujenga chuki unaposhauriwa kwa mambo mema.
- ❖ Kubali mashauri la sivyo utaanguka/ama kushindwa kabisa
- ❖ Kukosolewa na kushauriwa hakuondoi hadhi yako ya kuwa kiongozi, bali kunaimarisha uongozi wako.

**7. Tembelea Makanisa mengine ili kuangalia shughuli za Idara**

- ❖ Tembelea makanisa mengine upate changamoto wanazokutana nazo wenzako, fanya nao mazungumzo/kikao kidogo kubadilishana mawazo.
- ❖ Kutembelea vyama vingine kutaongeza na kuboresha mbinu na ujuzi katika utumishi wako.
- ❖ Unapopanga kutembelea vyama vingine, kumbuka kufuata taratibu za kanisa.

**8. Alika Vijana kutoka katika makanisa mengine**

- ❖ Alika vyama vinavyofanya vizuri katika makanisa mengine ya Waadventista Wasabato kuwatembelea na kuonesha program zao.
- ❖ Wanachama na washiriki waalikwe kuhudhuria program hizo.
- ❖ Mpango huu utasaidia kuamsha wanachama wako, na kujenga mahusiano mema miongoni mwa vijana.

9. **Uwe mtu wa kupatikana.**

- ❖ Mafanikio ya chama hutegemea sana upatikanaji wa kiongozi.
- ❖ Kiongozi anayepotea muda mrefu bila kuacha mipango pevu kwa viongozi wenzake, hawezi kufanikiwa katika uongozi wake.

10. **Omba msamaha unapokosea.**

- ❖ Ombi la dhati la msamaha ni jawabu la ghadhabu zote.
- ❖ Kuomba msamaha hakushushi hadhi kiongozi, badala yake kunaimarisha uongozi wako.

11. **Uwe mtu wa shukrani.**

- ❖ Washukuru wanachama kwa kila program au kazi wanayoifanya kwa ajili ya maendeleo ya kanisa au kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzao.
- ❖ Hilo litawatia moyo kuhudhuria tena watakapoombwa kufanya hivyo.

12. **Uwe mtu wa kiroho**

- ❖ Kazi ya uongozi inafanywa kwa maombi mengi na kwa kusoma neno la Mungu na Roho ya unabii.
- ❖ Wakati mwingine itakulazimu kufunga na kutenga muda maalum wa kujiombea nafsi yako na wale unaowaongoza.
- ❖ Mara zote viongozi wanaojali mambo ya kiroho ndio wanaofanikiwa.

13. **Uwe mtu wa kuaminika**

- ❖ Kwa wanachama, washiriki na kwa wazazi
- ❖ Kiongozi umepewa dhamana kubwa na ya thamani.
- ❖ Uwe na lugha nzuri kwa wanachama na watu wote.
- ❖ Timiza ahadi zako kwa wanachama na kwa kanisa.
- ❖ Tunza siri za wale unaowaongoza
- ❖ Simamia kwa uaminifu mali au fedha za wanachama
- ❖ Usifanye chama kuwa mtaji wa kujinufaisha binafsi. *Mfano; wakati wa kambi za vijana, safari au ziara za mafunzo* zinazofanyika nje ya kanisa mahalia.

14. **Uwe mvumilivu na asiyekata tamaa.**

- ❖ Uongozi sio kitu rahisi. Utakutana na mambo magumu na yanayokatisha tamaa. Mfano; *Dharau, kusemwa vibaya au kusingiziwa, mwitiko*

*mdogo katika kutekeleza mipango, upinzani wa makusudi wa wale wanaodhani ya kuwa wanajua zaidi kuliko wewe, n.k*

- Ikiwa kuna minong'oni mibaya inayosemwa juu yako irekebishe na kuacha. usiyotenda yasikukatishe tamaa. Endela na kazi ya Mungu.

**15. Uwe mbunifu.**

- Utendaji mkubwakatika idara ya vijana inahitaji ubunifu wa mambo na mipango.
- Jiulize maswali, nifanye nini ili vijana waone, waguse, watende, waweze kulielewa somo na kulifanya lidumu katika bongo zao?
- Wataalamu wanasema, kiongozi mzuri ni yule anayeshirikisha milango mingi ya fahamu.

**16. Furahia mafanikio ya wengine**

- Wanachama wana talanta na karama mbalimbali wengine wanakuzidiwewe kiongozi. Watie moyo, furahia kazi zao na wafungulie milango ya utumishi.
- Usiwaonee wivu na kuwadharau.

**17. Gawa madaraka**

- Kiongozi mzuri ni yule anayegawa madaraka kwa wale anaowaongoza, na kuwaamini kwamba wanaweza.
- Kugawa madaraka kutaifanya kazi yako iwe rahisi.
- Kugawa madaraka ni kuwaandaa wengine kuwa viongozi bora baada ya uongozi wako kumalizika

**18. Uwe mtu wa mawasiliano**.

- Kuna usemi usemao kuwa "Mawasiliano ni nguvu" (Communication is power)
- Hakikisha wanachama wanajua mipango yote ya chama mapema, taarifa za mikutano nje na ndani ya kanisa.
- Hakikisha wanajua viingilio na gharama za usafiri, zikiwemo zile za chakula na malazi mapema
- Fanya ufuatiliaji wa karibu kwa kuwakumbusha mara kwa mara

- Toa taarifa unaposafiri kwa muda mrefu na waeleweshe wanachama mipango inavyoendelea usipokuwapo.

**19. Fanya urafiki na wanachama wote.**

- Kiongozi bora ni yule ambaye anawapenda wanachama wote katika hali ya usawa, bila kujali kabila, rangi au aina ya familia anayotoka
- Kiongozi bora ni yule anayewaona wale anaowangoza kuwa ni watahiniwa wa mbinguni, na hivyo ana wajibu wa kuwahudumia wote kimwili kiakili na kiroho katika hali ya ulinganifu.

**20. Watembelee wanachama.**

- Kutawafanya wajisikie kuwa unawajali na kuwapenda.
- Kutawafanya wakueleze changamoto za maisha yao ili uwaombee
- Kutakusaidia kufahamu maeneo mbalimbali wanayoishi wanachama wako.
- Kutaongeza idadi ya wanachama.
- Kutakuimarisha katika imani.
- Kutalifanya kanisa liione kazi yako.

**“Pasipo nguvu kutoka kwa Baba juu mbinguni haya hayawezekani”**